

SOMO LA 2

BIBLIA: JINSI ILIVYOTUJIA

Kama ilivyoonyeshwa katika somo lililotangulia, BIBLIA ni kitabu cha kipekee. Kwa msimamo wowote ule, iwe ni kwa upande wa ujumbe, uthabiti au kutegemewa kwake kwote, au labda kwa namna ya kazi yake ya fasihi au thamani yake ya kihistoria, maandishi yake ya kale na muda mrefu ambao umepita, kweli ni kitabu cha ajabu. Unapofanya utafiti wa kina wa Biblia, inafaa kuwa na maarifa haya, historia na chanzo cha Biblia ya Kiingereza (hadi ifikie ya Kiswahili). Miswada ya mwanzo kabisa ya Biblia yenye pumzi ya Mungu haikuandikwa kwa lugha ya Kiingereza, bali ilikuwa katika lugha za Kiebrania na Kiyunani. Toleo linapokuwa halikaribiani na mswada wa asili, kulingana na wakati na lugha, hapo ndipo kazi ya mwanadamu huingilia kati, kwa sababu kazi ya kutuma ujumbe wa Biblia kutufikia kutoka wakati ule mpaka sasa kwa lugha yetu imetegemea watu ambao hawakuongozwa kwa Roho Takatifu. Ingawa mchango wa mwanadamu ni wa muhimu katika kazi hii kuu, yafaa tutambue ya kuwa toleo la Kiingereza la Biblia, kwa bahati mbaya, sio kazi safi ya Neno la Mungu, hata kama kuna matoleo mengine ambayo ni ya kiwango kikubwa cha usahihi.

LENGO LA SOMO LA 2 - 4

1. Kutoa muhtasari wa kazi ya kuvutia ambayo imechukua muda mrefu kwa Biblia kuweza kutufikia katika hali iliyomo, ili tupate kuielewa vema;
2. Kutoa habari ya kimsingi kuhusu historia na muundo wake;
3. Kusaidia kutambua aina na matoleo mbalimbali, na jinsi ya kuweza kutambua toleo lipi lina kiwango kikubwa cha usahihi ikilinganishwa na matoleo mengine kutokana na kazi ya asili; na kuelewa umuhimu wa kuangalia matoleo mengine kwa minajili ya ulinganifu.
4. Kuelewa umuhimu wa kuangalia kazi ya uandishi katika lugha ya Kiebrania na Kiyunani, konkodansi na kamusi, n.k, ili kuweza kuvuka vizingiti vya lugha ya Kiingereza kuhusiana na maneno yaliyotumiwa asili kama yalivyokusudia katika kazi ya Mungu na waandishi walioongozwa kwa pumzi yake.

BIBLIA ILIANZA LINI NA VIPI?

Sehemu kubwa ya Agano La Kale inachukuliwa na vitabu vitano vya kwanza. Musa ndiye anayepewa sifa za kuviandika vitabu hivyo na pia kitabu cha Ayubu. Hii inatupa tarehe ya uandishi wa Biblia, kwani, ingawa yaliyoandikwa na Musa yanaanzia miaka 4000 kabla ya kuja Masihi, aliishi nyakati za miaka ya 1570 hadi 1450 kabla ya Masihi, na katika muda wake wa miaka 120 aliyoishi (hasa kuelekea mwisho, labda 1500 kabla ya Masihi), twaweza kusema ndio mwanzo wa kupata ujumbe wa Mungu kwa njia ya uandishi.

Ujuzi wa kuandika haukuwa umeenea siku zile. Ushahidi wote waonyesha ya kuwa uandishi katika lugha ya Kiebrania haukuendelezwa hadi kufikia mwaka wa 1000 kabla ya Masihi au wakati wa Samweli na Mfalme Daudi. Njia mbadala wa uandishi ulikuwepo kabla ya hapo, njia

hizo za uandishi za kibabeli, Kikaldayo na Kimisri zimegunduliwa. Bila shaka, Musa alijifunza uandishi akiwa Misri.

Kifungu katika Biblia kinachotupa fununu kuhusu maandishi ya mwanzo kinapatikana katika Waamuzi 5:14 (pembezeni), ambapo wimbo wa Debora yazungumzia “fimbo ya mwandishi” (1250 kabla ya Masihi). Samweli, Daudi, Nathani nabii, nabii Gad, na wengine wengi wanasemekana waliyaandika mambo yao. Lakini mambo ya uandishi yalifunguka kabisa wakati wa uhamisho (kipindi cha Nehemia - Ezra mwaka wa 500 kabla ya Masihi), wakati ambapo walirekodi sherehe, wakaandika historia, walipanga maandishi ya unabii, na kujichagulia nyimbo za Zaburi kwa faida yao na ile ya vizazi vitakavyofuata. Matokeo ya juhudi hii ilikuwa ni mkusanyiko wa kuchukuliwa kama hazina ya thamani ya ujumbe wa Mungu. Ni mkusanyiko huu ambao Kristo na mitume walichukulia kama “maandiko” au “Musa na manabii.”

KUHIFADHI BIBLIA

Palitokea hatari nyingi ya kuweza kuendelea kuwepo kwa miswada hiyo ya mwanzo. Hati yoyote iliyoandikwa kwenye “papyrus” au ngozi ingeweza kupotea, kuangamizwa au kuchakaa kutokana na kupitwa na wakati. Twajua matokeo ya matumizi ya vitabu kwa muda wa miaka 10 au 20 tu kama vile matumizi ya Biblia zetu; twaweza kufikiria kwa urahisi matokeo ya kupitia kwa miaka 100 – kitabu kitakuwa kimezeeka na kupasuka ni rahisi, bora kiguswe tu. Kwa hivyo, ili kuhifadhi mswada na kuutumia kwa muda mrefu, kazi ya kunukuu kwa mikono iliendelea pasi na kukoma.

Miswada ya asili imetoweka kwa muda mrefu sasa lakini kuna matumaini ya kupatikana kwa vipande vya miswada hii. Makabila ya Israeli yalipohamishwa na Nebukadneza (Mfalme wa Babeli) na Antioku Epifane (Mfalme wa Misri) katika karne ya 6 Kabla ya Masihi, walihama na kubebana na nakala za maandiko hadi Babiloni na Misri.

Nakala hizi na hasa zile zilizoweza kufika Misri - zilitumiwa baadaye kama mianzo ya miswada na matoleo.

UDUMISHAJI WA USAHIHI NA UADILIFU WA BIBLIA

Mbali na kuangamizwa, palikuwepo na hatari ya makosa kujipenyeza katika kazi ya maandishi, wakati wa kunakili na kuchapisha. Makosa mengi hayakukusudiwa na yalitokea kwa ajali tu. Hebu tuonyeshe ni kwa namna gani – jaribu kunukuu hasa kurasa chache za kazi yoyote ya uandishi, utaona jinsi utakavyokosea hapa na pale. Makosa mengi ya uandishi yamekuwa ni ya aina hii – yaani, kijali na sio ya kukusudia. Ingawa, makosa machache, yametokea pale ambapo anayenukuu anajaribu kurekebisha kauli au kutumia maneno ya kurembesha maneno, au – na hii ndiyo hufanyika mara nyingi – hufanya kauli fulani ioane na dhana ya kidini ya yule mnukuaji na katika kizazi cha wakati anaoishi.

Kwa njia hii, tofauti ya matokeo katika uandishi yameonekana katika miaka ambapo nakala hizi zimetokea. Lakini shida hii si kubwa kama tunavyowazia, kwa sababu kuna watu walio jasiri wasiojua kinachoweza kufanyika, na kwa hivyo nakala yoyote ikiundwa au toleo likichapishwa, walihakikisha kuhifadhi maandishi kama yalivyokuwa mwanzoni kwa kutumia miswada ya asili waliyoweza kuipata wakati huo.

Nyingi ya miswada hii ingalipo hata leo, nyingine imehifadhiwa kwa zaidi ya miaka 2000. Ingawa sio nukuu za waandishi halisi wa Biblia, wametuletea Biblia kwa namna ambayo ni sahihi na hali ya kuweza kusomwa vema.

MATATIZO YA UTAFSIRI

Lugha ya Kiebrania ni lugha ngumu sana kutafsiri. Haina irabu /vokali. Anayesoma au anayetafsiri ndiye anaingiza mwenyewe. Alifabeti ya Kiebrania ina konsonanti 22. Kwa mfano, twaweza kuwa na neno la Kiebrania lenye konsonanti b d. Neno hili litakuwa ni bud, bad, bed au bid. Irabu italazimika kuongezwa na msomaji ili kukamilisha neno linalohitajika. Pia (na hili linapatikana kwa miswada mingi ya Kiyunani ya Agano Jipya na ile ya Kiebrania ya Agano la Kale) hapakuwepo na nafsi ya kutenganisha neno moja na jingine; hakuna uakifishaji, wala vifungu au milango/ sura. Hebu tuchukue mfano wa moja kwa moja kutoka kwa Kiebrania na tujaribu kutafsiri kwa Kiingereza au Kiswahili. Kazi ya mwanzo ni rahisi na imetekelezwa tayari – kutoa maneno ya Kiingereza au Kiswahili kwa yale ya Kiebrania. Yatokea hivi: “Yhrhthhsrchnndndknwnm;” au (kwa irabu na kutenganisha neno) “Yahveh thou hast searched me and known me” – “Yhvhnjmmnknfhm” “Yahveh umenijua mimi na kunifahamu.”

Wayahudi walijua tatizo hili, hasa kipindi kile cha uhamishoni, watu walipokuwa na maangiliano ya karibu na lugha ya kiyunani na kupunguza matumizi ya lugha ya Kiebrania. Waliokuwa na wasiwasi sana walikuwa ni watu wa kikundi cha Wayahudi waliojulikana kama MASORITE – “MASSORITES” (“Wahifadhi” au “walinzi” wa mambo ya jadi) ambao wajibu wao mkuu ulikuwa ni kuhifadhi maandishi na kuhakikisha herufi na matamshi hayabadilishwi. Kuhifadhi matamshi pasipo na irabu ni kazi ngumu mno, kwa hivyo wakabuni ishara za vokali ili kuingiza hati ya konsonanti mahali mwafaka, na wakaongezea ishara na uakifishaji. Waliianza kazi hii mwaka wa 500 baada ya kuwepo Masihi na ikaendelea kwa uvumilivu mkubwa na kujitolea mhanga kwa vizazi vingi. Mtindo huu wa ishara ulikamilika mwaka wa 900 Wa kuwepo Masihi – kipindi cha miaka mia nne! Hili ni jambo la kuvutia na kutia moyo sana katika somo hili, Kazi ya ajabu na muda ambao umetumiwa ili kujaribu kuhifadhi, kunakili na kutafsiri BIBLIA.

Kulikuwepo na matoleo na miswada tele iliyotumiwa na watafsiri kama vifaa vya kutafsiri Biblia tulizo nazo leo. Katika sehemu inayofuata tutaangalia kwa muhtasari miswada hiyo moja baada ya nyingine.

MSWADA WA KIEBRANIA

Hii ni miswada ya asili kabisa iliyokuwa na maandiko ya Agano La Kale kama ilivyoandikwa na waandishi walioongozwa na Roho Takatifu. Haipo kwa leo.

TOLEO LA WASAMARIA

Ingawa yaitwa “toleo,” yaani tafsiri kutoka katika lugha moja hadi nyingine, inafaa hasa iwe ni “marudio” ya kazi ya awali ya Kiebrania. Kazi ya marudio ya kudurusu, ni kutoa tena toleo ukitumia miswada iliyopo ili kutafsiri maandishi kwa kiwango na mwongozo wa udurusu. Iliandikwa na Wasamaria, watu ambao waliletwa katika nchi ya Palestina mnamo karne ya 7 kabla ya Masihi na mfalme wa Ashuru ili kujaza pengo la wale waliokuwa wamehamishwa Ufalme wa Israeli ulipoanguka na watu kwenda uhamishoni (2 Wafalme 17:24) Wasamaria walikuwa ni mchanganyiko wa mataifa kadhaa kutoka maeneo ya Ashuru. Walikuwa na chuki kuu kwa Wayahudi (ambayo ilieleweka pande zote mbili), lakini walijitia kumwabudu Mungu wa Waisraeli. Biblia ya Kiyahudi ilikuwa na sehemu fulani ambayo hawakuikubali, kwa hivyo walinukuu sehemu kutoka kwa Biblia ya Kiyahudi sehemu ile waliyoikubali tu - vitabu vitano vya Musa. Kwa kuwa lugha na maandishi ya kisamaria zilifanana na zile za Kiebrania, nakala ilikuwa sawa na ile ya asili.

Toleo la Wasamaria liliandikwa mwaka wa 400 kabla ya Masihi, miaka 100 tu baada ya Biblia ya Kiyahudi kuwepo. Chuki ya Wasamaria kwa Wayahudi iliwafanya wayalinde maandiko yao dhidi ya maingilio ya Wayahudi; Wayahudi nao wakafanya vile vile na miswada ya Kiebrania – haya yalichangia katika usahihi wa hali ya juu. Kama ilivyo na miswada yote, nakala mpya ililazimika kuundwa kutokana na ya kale ili isitoweke kwa kuzeeka au kuchakaa, au kwa kuangamizwa kabisa na maadui. Mswada mkongwe kabisa wa kisamaria uliopo leo ni nakala ya mwaka wa 1000 ya kuwepo Masihi. Ilipotelea katika nchi za Ulaya kwa muda lakini ikagunduliwa mwaka wa 1600 ya kuwepo Masihi.

TOLEO LA WAZEE SABINI

Wakati wa uhamisho wa Wayahudi, nchi ilipokuwa ikikaliwa na Waashuru, Wamede na Waajemi, Wayahudi wengi walikimbilia Misri, na bila shaka walichukua maandiko ya Kiebrania pamoja nao. Baada ya miaka mamia kadhaa Wayunani nao wakashinda na kutawala chini ya Aleksandria Mkuu, matokeo ya ushindi huu yalikuwa ni kuanzishwa na kuenezwa kwa lugha ya Kiyunani kwa haraka sana katika nchi zilizoshindwa ikiwemo Misri, ikawa lugha ya kimataifa ya wakati huo. Katika mwaka wa 250 kabla ya Masihi, Misri ilikuwa na mfalme wa Kiyunani ambaye alitaka awe na nakala ya maandiko ya Kiebrania katika lugha ya Kiyunani. Matakwa yake yalivutia koloni ya Wayahudi katika mji wa Aleksandria, Misri kwani wao pia waliona faida ya kuwa na nakala ya toleo la Kiyunani, kwani lugha ya Kiyunani ilikuwa na athari ya kuvutia kuliko ya Kiebrania.

Inavyosimuliwa, kamati ya wazee 72 wa kiyahudi ikaundwa, wataalamu katika lugha ya Kiebrania na Kiyunani wakaanza kazi ngumu lakini wengine wakaja kuhitimisha. Mchakato wote ulichukua miaka 200, kazi hii ikakamilika mwaka wa 50 Kabla ya Masihi. Matokeo ya kazi yao ilikuja kujulikana kama Toleo La wazee Sabini – SEPTUANGINT VERSION! Ikawa sana ya kudumu katika masinagogi ya wale walionena Kiyunani. “Septuagint” inamaanisha “Sabini.” Ingawa inadhaniwa kuwa Kristo alizungumza na kutumia Biblia ya Kiebrania, ni jambo la muhimu kuwa na tafsiri hii ya mwanzo ya kiyunani ili kulinganisha na kupimia usahihi wa nakala zingine na tafsiri ya Biblia za tangu hapo. Toleo hili “Septuagint” ni kwa heshima ya wazee Sabini na mbili wa Kiyahudi walioanza kazi hiyo. Jina hili huwekwa hivi katika tarakimu za Kirumi – LXX – 70

MISWADA YA AGANO JIPYA KWA KIYUNANI

Haya yalikuwa ni maandishi ya mwongozo wa Roho Takatifu ya mitume iliyoenezwa kwa waumini katika karne ya kwanza na ya pili kama ilivyo miswada ya Kiebrania, haipo kwa leo. Ilitafsiriwa mara moja na kusambazwa katika ndimi zingine – Kimisri, Kiethopia, Kiarmenia, Kilatini, na Kisiria – kwa msemu mwingine, katika lugha na lahaja sehemu ambazo lugha ya Kiyunani haikuwa inajulikana sana.

TOLEO LA MISRI

Hili likawa la muhimu pale ambapo injili ilienea hadi kwenye mto Nile kutoka mji wa Aleksandria. Ya kwanza ilikuwa ni toleo la SAHIDIKI (SAHIDIC) iliyoungwa mwaka wa 200 Baada ya Masihi. Ya pili ilikuwa ni toleo la KOPTIKI (COPTIC) iliyoungwa mwaka wa 250 baada ya Masihi na bado inatumika na Wakristo wa Kikoptiki wa nyanda za juu za Nile na sehemu za pwani za Mashariki ya kati.

Mungu ametupa neno lake kwa sababu Anataka tuwe wake. Njia ya kuwa Wake, imefunuliwa – kupitia kwa Yesu – Masihi – Mwana wa Mungu. Kujifunza mambo haya kutakuwezesha upate mwili usioweza kufa – mwili wa kutokufa – na uweze kutawala nchi wakati ambapo Masihi atarudi kuwaokoa Israeli kisha awe mfalme wa Israeli. Halafu Mungu ataimarisha Ufalme wake duniani na atawale ulimwengu kupitia kwa Mwanawe kwa muda wa miaka elfu moja. Ili kujiandaa kwa hili, yafaa kusoma mambo haya, tuyaamini na tubatizwe. Tafadhali yaweke haya akilini unapoendelea kupitia masomo haya.

MASWALI KWA SOMO LA 2

1. Miswada ya asili ya Biblia iliandikwa katika lugha mbili zipi?
2. Taja mambo manne ambayo twatarajia kuyatimiza katika masomo 2-4.
3. Nini maana ya neno “mswada”?
4. Tarehe gani ndiyo ya mwanzo katika uandishi wa neno la Mungu kwa njia ya uandishi?
5. Ni hatari gani ya nje ilikabili kuendelea kuwepo kwa Neno la Mungu?
6. Ni hatari gani mbili zilitishia kuharibu usahihi wa Neno la Mungu?

7. Je, miswada asili ya maandiko ya Roho Takatifu yapo?
8. Ni shida gani iliwakabili Watafsiri kutoka kwa lugha ya Kiebrania?
9. Ni sehemu gani ya Biblia imo katika toleo la Wasamaria?
10. Toleo la Wasamaria liliandikwa lini?
11. Nini kilisababisha kuandikwa kwa toleo la Wazee Sabini?
12. Kwa nini toleo la Wazee Sabini ni la maana kwa leo?
13. Nini maana ya “Marudio”?